

Ujumbe kutoka kwa Bi. Irina Bokova, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO, katika Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi, Februari 11, 2017.



Siku hii ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi ni fursa kwa watu wote kusimama pamoja na wasichana na wanawake katika sayansi.

Wasichana wameendelea kukabiliwa na ubaguzi na vikwazo vya kijamii na kiutamaduni, haya yote yakipunguza upatikanaji wa elimu na fedha kwa wasichana na wanawake kwa ajili ya utafiti na uwezo wa kufanya maamuzi. Hali hii hufunika jitihada zote za kufikia malengo ya Agenda ya Maendeleo Endelevu ya 2030 na Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Paris - haya yote huonyesha majukumu muhimu ya usawa wa kijinsia na sayansi.

Wakati huo huo, wasichana na wanawake ndio wanaobeba mizigo mizito zaidi ya umaskini na kukosekana kwa usawa, wao ndio wanaosimama katika mstari wa mbele kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, ikiwa ni pamoja na matokeo ya majanga ya asili. Waathirika wakuu wakiwa ni wasichana na wanawake wanaoishi katika maeneo ya vijijini na yale yaliyoko pembezoni.

Mafanikio halisi yanapaswa kuanza na haki na uthamini wa hadhi ya wanawake kwa kulea fikra na ubunifu wao. Ujumbe huu alitumwa wakati wa mikutano miwili iliyopita ya Wanachama wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (United Nations Framework Convention on Climate Change - COP 21 & 22). Ubinadamu hautomudu kupuuza nusu ya fikra zake za ubunifu.

Wasichana na wanawake hawana budi kuwezesha katika kila ngazi, katika kujifunza na utafiti, kutoka katika fani ya utawala hadi kufundisha, katika vitengo vyote vya kisayansi. Lengo hili linatilia mkazo Ilani, Wanawake katika Sayansi', ambayo ilizunduliwa mwaka jana na UNESCO pamoja na L'Oréal Foundation, inayolenga kuzihusisha serikali na wadau wengine katika kukuza ushiriki wa wasichana na wanawake katika sayansi. Tunapaswa kuwahamasisha wasichana na wanawake vijana wanasayansi kwa kutoa fursa na ushauri kwa vijana wanawake wanasayansi ili kuwasaidia kukuza taaluma zao. Tunapaswa kuongeza ufahamu juu ya kazi za kisayansi za wanasayansi wanawake na kutoa fursa sawa za ushiriki wao na uongozi katika wigo mpana wa vyombo vya ngazi ya juu vya kisayansi na matukio mengine ya kisayansi.

Ulimwengu unahitaji sayansi na sayansi inahitaji wanawake. Tunamkaribisha kila mmoja kutia saini ilani hii. <http://www.forwomeninscience.com/en/manifesto>. Pamoja, tunaweza kuleta mabadiliko.